# SHULE YA UPILI, MARANDA

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## KITANGULIZI MWIGO, 2024

**102/2** **Kiswahili - Lugha** **Karatasi ya 2**

**Machi, 2024** **Saa 2½**

Jina: ........................................................................ Nambari: ...........................

Mkondo: ............................. Sahihi: .................

**Maagizo**

*(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(b) Andika mkondo wa kidato chako kisha tia sahihi yako na uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*(c) Jibu maswali **yote.***
*(d) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
*(e) Majibu yote **sharti** yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
*(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*
***(g) Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.***
***(h) Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.***

---

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |

 ©Kamati Andalizi ya Mwigo wa Maranda – 2024

CamScanner

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Nimekaa na kutafakari kwa kipindi kirefu, juu ya mabilioni ya pesa ambayo yametengwa na serikali ili kudhamini miradi ya maendeleo ya wanawake. Kina mama au wanawake wengi wanakiri na kusema kwamba fedha hizo zimewezesha kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji kutoka kwa waume zao, kwani kila mmoja anamheshimu mwenzake kwa sababu ya kipato alicho nacho. Wengi wameweza kuanza biashara ndogondogo ambazo huwaletea angaa kipato kidogo.

Ukweli ni kwamba fedha hizi zimesaidia kuwatoa wanawake wengi katika unyanyasaji, kwani wengi wanaweza kuanzisha kazi za ujasiriamali na hata kuendesha shughuli mbalimabali za maendeleo.

Kutokana na mafanikio haya, wabunge waliopitisha hoja bungeni ya kuanzisha mpango huu wa kuwakwamua wanawake kimaendeleo wanafaa kupongezwa. Mafanikio haya yamewafanya akina mama kujikimu kimaisha na hivyo kutowategemea wanaume katika kila jambo.

Ukitaka kujua ukweli kuhusu hili, nenda kwenye masoko utaona akina mama jinsi wanavyohangaika na biashara zao. Kwa hivyo, ujasiriamali huendelezwa na akina mama zaidi na hivyo wanapaswa kuwezeshwa kwa kila hali na mali.

Akina mama pia wanafaa kupongezwa kwani wameamua kujitosa kukopa fedha kutoka kwenye taasisi mbalimbali za fedha. Fedha hizo kwa kiwango kikubwa zimewainua kutoka katika ufukara uliokithiri hadi katika maisha ya heshima. Wale ambao hawajajaribu kuchukua mikopo, ni muhimu wafanye hivyo ili wajikimu kimaisha.

Maisha ya sasa ni magumu, hivyo yanahitaji kusaidiana kwa kila hali na mali. Wanaume kwa wanawake ni vyema wachange bia ili wazumbue riziki. Ushirikiano utarahisisha maisha yao.

Hata hivyo, sio tu akina mama hao wameondokewa na unyanyasaji waliokuwa wakiupata ndani ya nyumba zao, toka kwa akina baba, bali hata masuala ya mrundikano wa kesi za kugombea ardhi kwa akina mama, zimepungua. Sababu ni kwamba akina mama wengi wameweza kujitafutia ardhi wenyewe kwa fedha walizonazo.

Ukweli ni kwamba hali imebadilika. Kinyume na hapo awali, ambapo majumba ya kifahari na mashangingi yalikuwa hifadhi ya wanaume, siku hizi wanawake wanamiliki hayo yote.

**Maswali**

1. Taja dhamira mbili za makala haya. (alama.2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

2. Eleza ni kwa nini msimulizi anawapongeza wabunge. (alama.2)

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

CamScanner

3. Wanaume walikuwa wakirudisha nyuma maendeleo nchini kivipi ? (alama.2)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

4. Sera za sekirali zimesaidia wanawake kivipi ? (alama.3)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

5. Eleza kwa nini baadhi ya wanawake wanaishi katika lindi la umasikini kulingana na makala haya. (alama.3)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

..............................................................................................................

6. Eleza maana ya msamiati na mafungu yafuatayo kama yalivyotumika katika makala haya : (alama 3)

(a) kutafakari

..............................................................................................................

(b) kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji

..............................................................................................................

(c) riziki

..............................................................................................................

**2. UFUPISHO**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Uwezo wa kuyakumbuka mambo ni hazina kuu kwa mtu yeyote yule aliye hai. Uwezo huu wa kukumbuka ni mojawapo ya shughuli changamano za ubongo. Ubongo wa mwanadamu hutekeleza shughuli hii kwa namna tatu. Kwanza, ubongo ukiathirika kwa namna yoyote katika mojawapo ya njia hizi, basi uwezo wa kuyakumbuka mambo huvurugika.

Ingawa inaaminika kuwa uwezo wa kukumbuka hurithishwa kutoka kizazi kimoja kingine, wataalamu wa maswala ya kiakili wanabaini kuwa uwezo huu unaweza kuimarishwa. Uimarishaji huu huhitaji mikakati madhubuti.

Njia mojawapo ya kustawisha uwezo wa kukumbuka ni kupitia kwa lishe. Vyakula vilivyosheheni vitamini B vyenye amino asidi husaidia kuimarisha uwezo wa kukumbuka. Vyakula kama hivi ni mboga, nyama (hasa maini) bidhaa za soya, matunda, maziwa, bidhaa za ngano, samaki pamoja na mayai. Vyakula vingine muhimu katika ustawishaji huu ni vile vyenye madini ya chuma. Madini haya huwezesha usambazaji wa hewa katika ubongo kwa wepesi. Vyakula ambavyo vina madini haya ni mboga za kijani, dengu, mawele, soya, matunda kama maembe, ufuta (simsim) pamoja na nyama, hasa maini na mayai.

Ubongo wa mwanadamu aliye hai hufanya kazi kila wakati, awe macho au amelala. Utendaji kazi wake huendeshwa na glukosi mwilini kwa hivyo vyakula vyenye sukari hii ni muhimu kuliwa. Hata hivyo, lazima mtu awe mwangalifu na kuhakikisha kuwa mwili una

CamScanner

kiwango cha sukari kisichohatarisha maisha. Haya yanawezekana kwa kula vyakula vyenye nyuzinyuzi kama vile mboga na matunda.

Njia ya pili ni kupiga marufuku vileo kama pombe na nikotini. Vileo hivi huathiri utaratibu wa kunasa, kuhifadhi na kutoa yaliyo ubongoni.

Iwapo mtu ana tatizo la kuyakumbuka majina ya watu, ni mujimu kufanya mazoezi ya kusikiliza kisha kurudia majina hayo wakati wa mazungumzo. Ni bora kulihusisha jina na sura ya mtu. Kwa njia hii ubongo utanasa na kuhusisha jina na kile kinacholengwa.

Woga na kuvurugika kiakili ni mambo mengine tunayopaswa kuepuka kila wakati. Ni kawaida mtu kupata woga wakati anapokabili jambo asilokuwa na uhakika na matokeo yake kama mtihani au mahojiano. Lakini anapaswa kuwa makini. Woga huo usikiuke mpaka na kuvuruga akili. Vurugu hizi huathiri kilichohifadhiwa ubongoni na namna ya kukitoa.

Hali kadhalika mwili wenye siha nzuri huhakikisha kuwa ubongo ni timamu. Wataalamu wengi wa siha wanakubali kuwa mazoezi ya kunyoosha viungo hustawisha na hivyo kuhakikisha kuweko kwa uwezo wa kukumbuka mambo. Ni muhimu kuwa na ratiba ya kunyoosha viungo kila wakati. Fauka ya haya mazoezi ya kiakili kama vile kusoma makala yanayovutia, kujaza mraba na michezo mingine kama mafumbo na vitanzandimi, ni muhimu katika kustawisha uwezo wa kukumbuka.

Jamii ya watu wenye uwezo wa kuyakumbuka mambo ni jamii iliyopiga hatua kimaendeleo. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuimarisha uwezo wa kukumbuka kila wakati.

(a) Eleza mchango wa chakula katika uimarishaji wa uwezo wa kukumbuka.

(Maneno 60 – 65) ( alama 5)

Matayarisho

..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................

Nakala safi

..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................

CamScanner

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

(b) Fupisha aya tatu za mwisho kwa maneno 70-80. ( alama 7 )

Matayarisho

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................



Nakala safi

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

CamScanner

**3. MATUMIZI YA LUGHA (AL 40)**
Soma na ujibu maswali yote kwa ufasaha

a) i.Tofautisha sauti zifuatazo (Al 4)
/l/ na /r/

............................................................................................

............................................................................................

ii.Taja vipasuo viwili vya kaakaa laini

............................................................................................

b) Ainisha silabi; **shughulika** (Al 2)

............................................................................................

............................................................................................

c) Weka shadda katika neno **mbuni** ili litoe maana mbili tofauti na ueleze maana hizo- (Al 2)

**i) mbuni** ............................................................

**ii) mbuni**............................................................

d) Weka maneno haya katika ngeli zake (Al 2)

i) Miwani ............................................................

ii) Wema ............................................................

e) Ainisha mofimu kaitka neno lifuatalo (Al 3)

alimketisha

f) Tumia kivumishi cha pekee katika sentensi kuonyesha umilikaji (Al 1)

............................................................................................

g) Yakinisha sentensi ituatayo katika hali ya mazoea (Al 1)
Hakuwasaidia kujibu maswali.

............................................................................................

h) Tumia neno **angika** pamoja na kinyume chake ili kutunga sentensi moja.(Al 1)

............................................................................................

i) Tumia nomino ya ngeli ya mahali dhahiri pamoja na kivumishi kirejeshi cha kati kwa sentensi. (Al 1)

............................................................................................

............................................................................................

CamScanner

j) Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha miundo miwili ya ngeli ya KI-VI.(Al 2)

..........................................................................................

..........................................................................................

k) Kanusha sentensi ifuatayo katika wingi. (Al 1)
Mwanafunzi huyo akisoma kwa bidii ataupita mtihani.

..........................................................................................

l) Tunga sentensi sahihi ukitumia kiunganishi cha kuongezea. (Al 2)

..........................................................................................

m) Ainisha vihusishi katika sentensi zifuatazo. (Al 2)
i) Tunu ni mrembo kama mama yake

..........................................................................................

ii) Watawasili kufikia juma lijalo

..........................................................................................

n) Andika methali moja inayoonyesha dhana ya kutodharau kitu chako. (Al 1)

..........................................................................................

o) Andika katika udogo wingi. (Al 1)
Kitabu cha mtu huyo kimeletwa na mwanafunzi wake

..........................................................................................

p. Tunga sentensi ili kubaini matumizi mawili ya kinyota. (al 2)

i. ..........................................................................................

..........................................................................................

ii. ..........................................................................................

..........................................................................................

q. Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo; (al 2)
Amewaletea mkate.

i. ..........................................................................................

ii. ..........................................................................................

r. Unda nomino mbili kutokana na kitenzi **imba**. (al 2)

i...............................................

ii...............................................

s. Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. (al 2)
'Nitaenda kumtembelea nyanya yake hapa mjini wiki ijayo.' Juma alisema.

..........................................................................................

CamScanner

..........................................................................................

t. Ainisha virai katika sentensi ifuatayo. (al 4)
Wanafunzi wote werevu walituzwa jana jioni.

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

u. Ainisha vishazi; (al 2)
Kalamu iliyonunuliwa jana imepotea leo.

..........................................................................................

..........................................................................................

**4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

i. Huku ukitoa mifano mwafaka, onyesha sifa tano za sajili katika muktadha wa utaalamu.

(al. 5)

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

ii. Onyesha njia tano ambazo kwazo Kiswahili kimeweza kuenea duniani tangu enzi za ukoloni hadi sasa. (alama 5)

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

..........................................................................................

CamScanner